


Programu za IEC zinahimiza ushirikiano wa jumuiya nzima ya shule kwa njia ya kushiriki katika matukio mengi ya shule.

| Shule | Anwani | Mawasiliano |
|---|---|---|
| **Shule ya Msingi** (PP hadi Miaka 6) | | |
| **Shule ya Msingi Eddystone** | Littorina Avenue, Heathridge 6027 | 9406 5100 |
| **Shule ya Msingi Koondoola** | 50 Burbridge Avenue, Koondoola 6064 | 9345 6200 |
| **Shule ya Msingi Nollamara** | 101 Harrison Street, Nollamara 6061 | 9413 1550 |
| **Shule za Msingi** (Mwaka 1 hadi 6) | | |
| **Shule ya Msingi Beaconsfield** | 5 Hale Street, Beaconsfield 6162 | 9432 1000 |
| **Chuo cha Msingi Dianella** | Laythorne Street, Dianella 6059 | 9263 5100 |
| **Shule ya Msingi Highgate** | 147 Lincoln Street, Highgate 6003 | 9253 2700 |
| **Shule ya Msingi Parkwood** | Zelkova Way, Parkwood 6147 | 9235 1411 |
| **Shule ya Mingi Thornlie** | 86 Thornlie Avenue, Thornlie 6108 | 9232 3480 |
| **Shule ya Vidato vya Juu** (Miaka 7 hadi 10) | | |
| **Shule ya Vidato vya Juu ya Balga** | 2 Markham Way, Balga 6061 | 9247 0219 |
| **Chuo cha Greenwood** | Coolibah Drive, Greenwood 6024 | 9243 9200 |
| **Shule ya Vidato vya Juu ya Lynwood** | 436 Metcalf Road, Parkwood 6147 | 9354 0600 |
| **Shule ya Vidato vya Juu ya Melville** | 18 Potts Street, Melville 6156 | 6274 1300 |
| **Shule za Sekondari za Vidato vya Juu ya Upili** (Miaka 11 na 12) | | |
| **Kampasi ya Vidato vya Juu ya Cyril Jackson** | 53 Reid Street, Bassendean 6054 | 9413 4720 |
| **Kampasi ya Vidato vya Juu ya North Lake** | 188 Winterfold Road, Kardinya 6163 | 9314 0444 |

Department of **Education**
GOVERNMENT OF WESTERN AUSTRALIA

# Vituo vya Kufundisha Kiingereza

## kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari


cc BY



# Je, Vituo vya Kufundisha Kiingereza ni nini?

Vituo vya Kufundisha Kiingereza (IECs) vimebobea kufundisha Kiingereza kama Lugha au Lahaja ya Ziada (EALD) kwa wanafunzi wapya waliowasili ambao wanastahiki kujiunga katika shule za serikali za Australia Magharibi. Wanafunzi wa IEC wanaotoka nchi mbalimbali zenye lugha na tamaduni tofauti, wanachangia katika mazingira ya shule yenye msisimko, uwezo na jumuishi. Mahudhurio katika IEC ni kwa hadi miezi 12 (au miezi 24 pale wanafunzi wanapokuwa na viza ya ukimbizi) kutegemeana na viza na mahitaji ya mwanafunzi.

Vituo vya Kufundisha Kiingereza vipo ndani ya shule za kawaida. Kuna vituo kumi na nne ndani ya shule za serikali katika eneo la mji mkuu wa Perth - nane katika shule za msingi, vinne katika shule za sekondari na viwili katika kampasi za shule za vidato vya juu.

Programu za IEC zinahimiza ushirikiano na jumuiya nzima ya shule kwa njia ya kushiriki katika matukio ya shule nzima ambayo yanajumuisha mwingiliano na safari ndogo za kielimu, matamasha ya michezo, matukio na mikusanyiko ya kijamii.

IEC za msingi huhudumia wanafunzi wenye umri wa miaka 5 hadi 11, pamoja na vituo vitatu vya msingi vinavyotoa madarasa ya Chekechea kwa wanafunzi wenye umri wa miaka 4 kutoka malezi ya ukimbizi. IEC ya pili huhudumia wanafunzi wenye umri wa miaka 12* hadi 16. IEC ya wakubwa huhudumia wanafunzi wenye umri wa miaka 16 na zaidi.

*Wanafunzi wanaoanza shule ya sekondari katika mwaka wa 7 wanaweza kuwa na umri wa miaka 11 kuelekea 12 kabla ya Julai mwaka huo.

## Faida za IEC

- Msaada na maelekezo makini ya ufundishaji maalum wa lugha ya Kiingereza ili kuongeza uwezo wa wanafunzi kupata mtalaa wa kawaida.
- Udogo wa darasa ambao unasaidia kujifunza kwa mtu mmoja mmoja.
- Msaada wa kitamaduni katika mazingira ya malezi.
- Walimu na wafanyakazi wasaidizi waliobobea.
- Huduma ya basi ya kila siku ya bure kwa watoto wenye umri wa shule ya msingi.
- Kupata huduma maalum za afya.

## Mtalaa katika IEC

Vituo vya Kufundisha Kiingereza vinatoa programu za kujifunza zilizoainishwa kutegemeana na Mtalaa wa Australia Magharibi.

Mtalaa katika IEC unalenga mahitaji ya kujifunza lugha ya Kiingereza ya wanafunzi mmoja mmoja. Ili kuwasaidia wanafunzi wafanye mabadiliko mazuri kwenye madarasa ya kawaida, masomo ya msingi ikiwemo Hisabati, Sayansi, Sanaa na Sayansi ya Jamii.

IEC huwasaidia wanafunzi kujifunza Kiingereza na kuwa na uelewa wa muktadha wa kitaaluma wa umri husika na wa kijamii wa shule za Australia Magharibi. IEC na shule za mahali husika hushirikiana ili kulinda mabadiliko mazuri kwenye shule za mahali husika.

## Wafanyakazi katika IEC

IEC huajiri walimu wa EALD na Wasaidizi wa Elimu ya Utamaduni (EEAs). Walimu wa EALD wana uzoefu na wamebobea kufundisha programu za EALD kuendana na umri, sambamba na Mtalaa wa Australia Magharibi. EEA wanazungumza lugha mbalimbali, ambazo zinaweza kujumuisha lugha ya kwanza ya wanafunzi wa IEC.

## Upatikanaji wa IEC

Sifa za kujiunga katika IEC kunategemea na masharti na yanaweza kujumuisha:

- Wanafunzi ambao wapo katika Mwaka 1 hadi 12 na ni wapya kujifunza Kiingereza, ikiwemo wale ambao walizaliwa Australia;
- Wanafunzi ambao wana viza za ukimbizi na wapo katika Madarasa ya Chekechea hadi Miaka 12; na
- Wanafunzi ambao wamerejea Australia baada ya kipindi kinachozidi miezi 6.

## Kujiunga katika IEC

- Wasiliana na IEC ya mahali ulipo ili kuweka miadi. (Angalia orodha ya IEC ili kupata kituo kilicho karibu zaidi)
- Taarifa ifuatayo inahitajika kwa ajili ya kujiunga:
  - ➔ tarehe ya kuwasili nchini Australia;
  - ➔ jina la mwanafunzi;
  - ➔ anwani ya sasa;
  - ➔ lugha/lahaja zinazozungumzwa nyumbani;
  - ➔ namba ya viza daraja dogo; na
  - ➔ maelezo ya mawasiliano.
- Ili kusaidia mchakato wa kujiunga, usafiri kwenda na kurudi kutoka IEC na huduma ya ukalimani vinapatikana bila malipo.

